# Kutembelea Uandaaji wa Video za Kitabu cha Mormoni

Na Urais Mkuu wa Msingi

Karibuni, tulitembelea mojawapo ya maeneo ambapo video mpya ya Kitabu cha Mormoni ilikuwa ikirekodiwa. Tulipata kutazama tukio ambalo Yesu Kristo aliwatembelea watoto mmoja baada ya mwingine.

Tulitazama watoto wakigusa mikono ya mwigizaji anayeigiza kuwa ni Yesu. Alizungumza nao kwa wema, upole, kama vile ambavyo Yesu angefanya.

Watoto walituambia kwamba kwa sababu ya uzoefu wao, ushuhuda wao wa Kitabu cha Mormoni ulikua na nguvu zaidi. Yesu *alikuja* kwa Wanefi. Yeye *aliwabariki* watoto. Hadithi ni ya kweli.

Unaweza ukajua hilo pia. Soma Kitabu cha Mormoni. Tazama video za Kitabu cha Mormoni. Unapofanya hivyo, unaweza kumkaribia Yesu. Wewe ni mpendwa Kwake. Na Roho Mtakatifu atakusaidia kuhisi upendo na amani ya Mwokozi. ●


Mwigizaji aliyeigiza Yesu alikuwa mwema na mpole.


Katika tukio hili, malaika waliinuliwa juu hewani kwa waya!


Msichana huyu alimsaidia mtu wa kamera kukaa vizuri.




Urais wa Msingi ulipenda kukutana na watoto kwenye uandaaji wa video.




Watoto wengi walikuwa kwenye video.

Unaweza kuangalia video za kitabu cha Mormoni katika ChurchofJesusChrist.org.

Ilikuwa kama nilikuwa naishi Kitabu cha Mormoni.
**Emoani W., miaka 11**

Ilinisaidia kujua kwamba Yesu aliwatembelea hawa watu.
**Isaac P., mika 7**

Wakati Yesu na Malaika wanatokea, Ilinifanya niwe na furaha.
**Lilly W., miaka 8**

Unaweza ukashiriki video na yeyote!
**Castle W., miaka 9**

Utajifunza zaidi pia kuhusu Yesu Kristo.
**Christina C., miaka 9**

Ilinifanya nijiulize itakuwaje tukikutana na Yesu.
**Rhett M., miaka 4**

